{«DateLetterGenerated»}

{«Guardian»}
{«MailAddress»}
{«MailCity», «MailState» «MailZip»}

Mpendwa {«Guardian»}:

Mnamo {«InterviewDate»}, mwakilishi wa {«HDName»} alizungumza nawe ili kujadili vyanzo vinavyowezekana vya mfiduo wa madini ya risasi wa mtoto wako. Ripoti iliyoambatishwa inaeleza athari za madini ya risasi kwa mtoto wako na inafafanua huduma iliyotolewa.

Yaliyoorodheshwa hapa chini ni baadhi ya mambo unayoweza kufanya sasa ili kupunguza mfiduo wa madini ya risasi wa mtoto wako:

- Osha sehemu kama vile vizingiti vya madirisha, fremu za madirisha na sakafu mara kwa mara.
- Safisha uchafu na vumbi kwa kutumia mfumo wa kuvuta vumbi wa High Efficiency Particulate Air (HEPA). Mashine ya kuvuta vumbi ya HEPA inapatikana kwa mkopo katika idara ya afya au shirika la makazi la eneo lako.
- Osha mikono ya mtoto wako, hasa kabla ya kula na kulala, na baada ya kucheza sakafuni au nje.
- Osha nguo, pajama na vidude vya kuchezea vya mtoto wako mara kwa mara.
- Mpe mtoto wako lishe bora yenye kiwango cha juu cha madini ya kalisi (kwa mfano, maziwa, jibini, tofu na mtindi) na madini ya chuma (kwa mfano, siagi ya karanga, mboga za majani, zabibu kavu na nyama ya ng'ombe) na kiwango cha chini cha mafuta (epuka vyakula vya kukaangwa). Mhimize mtoto wako ale mezani ili kuepuka uchafuzi wa chakula.
- Hakikisha mtoto wako anafanyiwa kipimo cha madini ya risasi ndani ya miezi miwili baada ya kipimo cha kwanza au kama ulivyoelekezwa na daktari wako ili kuona mabadiliko yoyote katika kiwango cha madini risasi kwenye damu.
- Usihifadhi juisi za matunda au mboga katika makopo ya chuma baada ya kopo kufunguliwa—tumia vyombo vya plastiki au glasi badala yake. Epuka kutumia vyombo vya kioo vilivyotengenezwa kwa madini ya risasi au vyombo vya ufinyanzi vilivyoingizwa nchini kutoka nchi za kigeni au vya zamani.
- Usiwaruhusu watoto wako kuchezea au kutafuna nyenzo zilizochapishwa kama vile magazeti au majarida—wino wa rangi unaweza kuwa na madini ya risasi.
- Usiwaruhusu watoto wacheze kwenye udongo wazi, hasa karibu na msingi wa nyumba. Tafuta maeneo yenye nyasi au nyenzo salama za kufunika udongo.

Maelezo ya ziada kuhusu madini ya risasi yanaweza kuombwa kwa kupiga simu kwa {«HDPhone»}.

Kwa Uaminifu,

{«HDRepresentativeName»}
{«HDRepresentativeTitle»}
{«HDName»}

Ripoti ya Muhtasari ya Kiwango cha Juu cha Madini ya Risasi Kwenye Damu

Ya: {«ChildFirst» «ChildLast»}
Tarehe ya Kuzaliwa: {«ChildDOB»}

Imeandaliwa Na:

{«NameofIndividualPreparingReport»}
{«TitleofIndividualPreparingReport»}

Sahihi:_____

{«HDName»}
{«HDStreetAddress»}
{«City, State Zip»}
{«HDPhone»}

Tarehe ya Ripoti: {«DateofReport»}

I. Mfiduo wa Madini ya Risasi

Madini ya risasi yanaweza kuharibu karibu kila mfumo katika mwili wa mwanadamu na yana madhara kwa watu wazima na watoto. Madini ya risasi ni hatari zaidi kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka sita kwa sababu ya ukuaji na maendeleo yao ya haraka. Athari mbaya zaidi ya mfiduo wa madini ya risasi ni katika ubongo unaokua wa mtoto. Matatizo yanayohusiana na mfiduo wa madini ya risasi yanaweza kudumu kwa maisha yote ya mtoto na yanaweza kuathiri uwezo wake wa kiakili, tabia na uwezo wa kujifunza. Ingawa hakuna kiwango cha madini ya risasi katika damu ya mwanadamu ambacho kimepatikana kuwa salama, viwango vya madini ya risasi ambavyo ni zaidi au sawa na mikrogramu 3.5 kwa desilita huchukuliwa kuwa vya juu na Kituo cha Marekani cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (US Centers for Disease Control and Prevention (CDC)) na hatua zinapaswa kuchukuliwa ili kujaribu kupunguza kiwango cha madini ya risasi cha mtoto hadi viwango vya chini kuliko mikrogramu 3.5 kwa desilita.

Watoto wengi wa Ohio walio na viwango vya juu vya madini ya risasi hupata mfiduo wa madini ya risasi kupitia vumbi la kawaida la nyumbani linalotokana na rangi ya madini ya risasi kubambuka na kubanduka ndani na nje ya majengo ya kabla ya 1978 wanayotumia muda mwingi ndani yake. Watoto wengine pia hupata mfiduo kutoka kwa madini ya risasi yanayoletwa nyumbani na wanafamilia ambao hufanya kazi wakitumia madini ya risasi au wanaofanya shughuli za kujifurahisha ambazo huwafanya kupata mfiduo wa madini ya risasi. Udongo uliochafuliwa pia ni vyanzo vinavyowezekana vya madini ya risasi. Maji kutoka kwa vyanzo vya kibinafsi na bidhaa nyingine zinazoingizwa nchini kutoka nchi za kigeni kama vile vidude vya kuchezea, vipodozi na viungo vya mapishi zimepatikana kuwa na madini ya risasi lakini hazihusishwi kwa kawaida na viwango vya juu vya madini ya risasi katika damu kwa watoto ndani ya Ohio.

{**«HDName»**} hupokea data kutoka kwa Idara ya Afya ya Ohio (Ohio Department of Health (ODH)) ambayo hupokea matokeo yote ya vipimo vya madini ya risasi ya wakazi wa Ohio, bila kujali umri au kiwango chao cha madini ya risasi. Mpango huu huwasaidia wanafamilia, watoa huduma wa matibabu na washiriki wengine wa jamii kupunguza na kuzuia mfiduo wa madini ya risasi. Mpango huu pia hutoa huduma ya moja kwa moja kwa watoto kuanzia wanapozaliwa hadi umri wa miezi 72 (miaka 6).

II. Mchakato wa Mahojiano

Wakati {**«HDName»**} inapofahamu kwamba mtu mwenye umri wa chini ya miezi 72 ana kiwango cha madini ya risasi ambacho ni zaidi au sawa na mikrogramu 3.5 kwa desilita, {**«HDName»**} hujaribu kufanya mahojiano na mzazi au mlezi wa mtoto ili kubaini vyanzo vinavyowezekana vya madini ya risasi katika mazingira ya mtoto.

III. Muhtasari wa Mahojiano

{**«HDName»**} ilipokea ripoti kwamba {**«ChildFirst» «ChildLast»**} alikuwa na kiwango cha madini ya risasi kwenye damu cha {**«BLLResult»**} **µg/dL** mnamo {**«DrawDate»**}. Mahojiano yalifanyika mnamo {**«DateofInterview»**} ili kutambua chanzo/vyanzo vinavyowezekana vya mfiduo wa madini ya risasi wa mtoto wako. Mahojiano yalifanywa na {**«InterviewerName»**}.

Wakati wa mahojiano, familia yako iliulizwa mfululizo wa maswali kuhusu mazingira na tabia za mtoto wako na hojaji ilijazwa (tazama nakala iliyoambatishwa). Ingawa {**«HDName»**} huenda imependekeza tabia au vitu fulani ambavyo huenda vimechangia mfiduo wa madini ya risasi wa mtoto, haiwezekani kutambua vyanzo halisi vya mfiduo wa mtoto bila tathmini kamili ya hatari ya madini ya risasi.

Nyenzo za elimu zimetolewa ili kukusaidia kupunguza vyanzo vya madini ya risasi katika mazingira ya mtoto wako. Tafadhali wasiliana na {**«HDName»**} kupitia {**«HDPhone»**} ikiwa una maswali yoyote kuhusu ripoti hii au taarifa iliyotolewa.